# IMAM HUSAIN NI MFUMO WA MAREKEBISHO NA MAGEUZI

الحسين منهج الإصلاح والتغيير

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimehakikiwa na:**
Shuaib Ayoub

ترجمة

# الحسين منهج الإصلاح والتغيير

تأليف

الشيخ حسن الصفار

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 063 – 0

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimehakikiwa na:**
Shuaib Ayoub

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Mei, 2014
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

IMAM HUSEIN (AS) NA HARAKATI
ZAKE ZA AMANI ........................................................................ 5

Utamaduni wa Amani na Utamaduni wa Mabavu .......................... 5

Maamkizi ya Uislamu ........................................................................ 8

Utamaduni wa Zama za Kimada .................................................. 14

Utumiaji Nguvu na Kutishiwa kwa Amani ya Jamii .................... 16

Amani ya Jamii Yetu Inaelekea Wapi? ......................................... 17

Baina ya Ukhalifa naUfalme ........................................................ 20

Husein na Mapambano ya Amani ................................................. 24

IMAM HUSEIN NA MFUMO WAKE
KATIKA KULINGANIA NA KUJADILIANA ............................ 26

Njia ya kuathiri wengine ............................................................... 26

Tatizo la Majadiliano Katika Jamii ya Kiislamu .......................... 31

Hali Gani hii ya Kutokuendelea? ................................................. 35

Dondoo Kutoka Katika Riwaya ya Imam Husein
(as) na Sira Yake ........................................................................... 38

Werevu wa Kukosoa ..................................................................... 39

Kuepukana na Mijadala Isiyo na Tija ........................................... 40

Kuamsha Utu, Dhamira na Maadili Yenye Uongofu: .................. 43

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *Al-Husayn Manhaju 'l-Islahi wa 't-Taghyiri* kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar. Sisi tumekiita, *Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi.*

Imam Husain (a.s.) ni mjukuu wa Mtume (s.a.w.w.) kutokana binti yake mpenzi Fatma Zahra (a.s.) na baba yake ni Imam Ali Ibn Abu Talib (a.s.). Imam Husain (a.s.) ni Imamu wa tatu katika Maimamu wa Ahul Bayt (a.s.).

Imam Husain (a.s) ni maarufu sana kutokana na muhanga alioutoa pale Karbala mwaka wa 60 Hijria. Kila mwaka inapofika mwezi wa Muharram, Waislamu kote ulimwenguni hufanya majlisi za kumbukumbu kwa ajili ya masaibu ya Karbala yaliyomfika mjukuu huyu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Imam Husain alifanya mageuzi makubwa na ya kihistoria katika ubinadamu; wala si kwa Waislamu tu bali kwa wanadamu wote kama utakavyoona katika kitabu hiki.

Kama ilivyo kawaida, Maimamu hawa wanaotokana na Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni wateule wa Mungu, maisha yao ni mfano wa kuigwa katika jamii ya wakati ule na wakati huu na wakati ujao.

Mwandishi katika kitabu hiki pamoja na mambo mengine anaelezea jinsi Imam Husain (a.s.) alivyoweza kuleta mageuzi na mabadiliko katika jamii ya wanadamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itra imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Abdul Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kutoka lugha yake ya asili ya Kiarabu kuja katika lugha ya Kiswahili, pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

# UTANGULIZI

Upepo wa mapinduzi na mageuzi unavuma katika jamii zetu za Kiislamu, na nchi za Kiarabu zinaishi katika msimu wa mapinduzi yenye kuchanua, humo yamemea matumaini ya wananchi wenye matarajio ya marekebisho na maendeleo. Umma ulibanwa mno na siasa za dhulma na ukandamizaji, hatimaye mateso yake yalizidi na kuongezeka kutokana na ufisadi na kubaki nyuma, na sasa unashangazwa na tofauti kubwa iliyopo baina ya hali yake na hali za wananchi ambao wananeemeka kwa demokrasia na wanafurahia haki za uraia.

Na baada ya nchi za kiarabu kukata tamaa ya kurejea kwa mwanga ambao uliinuliwa juu na mashujaa wa mapinduzi ya kijeshi na vyama vya mirengo ya kulia na kushoto, na kwa nembo za uongo ambazo serikali fisadi zimezitumia kujificha na kutenda uovu wake, sasa limejitokeza vuguvugu la wananchi katika nchi nyingi za kiarabu, vuguvugu ambalo liko mbali na fikra na nadharia, na liko nje ya udhibiti wa watu maarufu na viongozi, ili kutekeleza matakwa ya raia katika kufanikisha marekebisho na mageuzi, na kupiga vita dhulma na ufisadi.

Lakini nguvu za ubeberu wa kimataifa, na vituo vya ukandamizaji wa ndani, na nguvu ya wanamageuzi wasiofungamana na upande wowote na wenye mwelekeo potovu wa kuhodhi na wa maslahi binafsi, kama kawaida ya nguvu hizi na mielekeo hii, inakwenda mbio

kujiunga na wimbi la mapinduzi na mageuzi kwa lengo la kulipotosha na kulitoa wimbi la mapinduzi kutoka kwenye mwelekeo wake sahihi, na kulielekeza kwenye maporomoko ya ukatili na vita vya ndani vya wenyewe kwa wenyewe na katika madimbwi ya ikhitilafu na fitina za kimakundi.

Ili kukabiliana na hatari hizi na kulinda harakati za wananchi dhidi ya uvamizi na njama, ni haja ilioje kwa umma kuzinduka na kuamka, na kuiga mifano ya mageuzi elekezi na tajriba za mapinduzi ya kweli. Unapowadia kwetu msimu wa Ashura na kumbukumbu ya mapambano ya Bwana wa Mashahidi Abu Abdillahi Husein (as) bila shaka wakati huo ni fursa nzuri ya kukata kiu kutoka kwenye mfumo wake wenye kudumu, na kufaidika na mwanga wa mshumaa wake wenye kuangaza, ambao ni zaidi ya karne sasa tangu uwashwe lakini bado haujazima na haujazidisha isipokuwa mwangaza na kumeremeta.

Hakika Husein alitoka kwa ajili ya kwenda kufanya marekebisho katika umma kama alivyosema (as), naye ndiye yule aliyelelewa na wahyi na utume, na hivyo sira yake katika mapambano ya marekebisho ni mfumo unaoigwa, khutba zake na misimamo yake vinatengeneza mafunzo yenye kumwongoza kila aliye huru mwenye ghera juu ya maslahi ya umma wake na jamii yake. Hivyo kurasa hizi chache zilizoko mbele ya msomaji ambazo ni uhariri wa mihadhara miwili iliyotolewa katika msimu wa Ashura mwaka 1428 Hijiria, ni dondoo kutoka katika sira ya Husein (as), na inatoa mwangaza kutoka kwenye mfumo wake wa marekebisho ya kisiasa na mageuzi ya kijamii. Asaa katika kuzisambaza kutachangia katika kuimarisha utamaduni wa mwamko na kuzatiti misingi ya ujumbe na dini.

**Hasan Musa as Saffar**
**23 Shawwal 1433 Hijiria,**
**sawa na 10 Septembe 2012.**

بسم الله الرحمن الرحيم

# IMAM HUSEIN (AS) NA HARAKATI ZAKE ZA AMANI

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ

**"Enyi mlioamini! Ingieni katika usalama nyote, wala msifuate nyayo za Shetani. Kwa hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi." (Surat al-Baqarah: 208).**

**Utamaduni wa Amani na Utamaduni wa Mabavu:**

Mwanadamu kwa kuzingatia kuwa ni mwanajamii, huishi ndani ya mazingira ya jamii ambayo humlea na katika utamaduni unaomzunguka, na hivyo mambo mawili hayo hutoa mwelekeo wa nafsi yake na huathiri katika mwenendo wake. Kama atakulia katika jamii inayotawaliwa na huruma, upendo na mshikamano, hakika hali hiyo humwandaa kisaikolojia ili afuate njia ya amani, upendo na muamala sahihi katika maisha. Ama akikulia katika mazingira ya ubabe na ukatili, au ikiwa utamaduni uliotawala katika jamii yake ni utamaduni unaoshajiisha mabavu na ukatili, bila shaka jamii hii itatengeneza watu waasi, makatili na wababe. Na kwa sababu hiyo ndio maana Uislamu unahimiza kuandaa mazingira ya kijamii yanayozungukwa na huruma na upendo. Wazazi

wawahamasishe watoto kuwa na tabia ya upole na upendo, imepokewa katika hadithi kwamba busu la baba kwa mtoto wake lina malipo, katika hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Mwenye kumbusu mtoto wake Mwenyezi Mungu anamwandikia jema."[1] Na pia imepokewa kutoka kwake (saww) kuwa: "Zidisheni kuwabusu watoto wenu, hakika mnayo katika kila busu daraja katika pepo."[2] Na katika riwaya nyingine ni kwamba mtu mmoja alimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amemkalisha Hasan na Husein katika mapaja yake, na alikuwa anambusu huyu na kisha anambusu mwingine, yule mtu akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nina watoto kumi na sijambusu hata mmoja kati yao." Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema: "Mimi sina chochote kwako, kama Mwenyezi Mungu ameondoa huruma moyoni mwako."[3] Na katika kitabu Wasailus-Shia[4] kuna hadithi kwamba Mtume alisema: "Asiyehurumia hatahurumiwa."

Hivyo inapasa mtoto aishi katika mazingira ya upendo na upole tangu utotoni mwake. Na Uislamu unaamuru wanajamii wote wawahurumie watoto, na hii ni katika adabu ya Kiislamu na ni katika maelekezo yake matukufu kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): "Waheshimuni wakubwa wenu na wahurumieni wadogo wenu."[5] Hakika Uislamu unamtaka mwanadamu aishi katika jamii inayotawaliwa na huruma, na sio tu ndani ya familia bali katika jamii nzima, na kwa hiyo malezi haya yataakisi katika silka yake, na

1 *Wasailus-Shiah*, Juz. 21, Uk. chapa ya kwanza 1993 (Beirut: Muassasati Aalil- Bait lilihiyaai turaath), Uk. 485, Hadith namba 27655.

2 *Makarimul – Akhilaaq*, chapa ya ya pili 1422 Hijiria (Beirtut Muasastu al- Ilimiy), Uk. 211.

3 Rejea iliyotangulia , Uk. 220.

4 *Wasailus-Shiah*, Juz. 21, Uk. 485, hadithi ya 27657.

5 *Biharul- An'war*, Juz. 93, chapa ya tatu 1403 Hijiria (Beirut, Daru Ihiyaai Turathil- Islaamiy), Uk. 357.

utamuona anamheshimu huyu na anamhurumia yule, anaunga udugu wa jamaa zake na wala hawaudhi jirani zake.

Na katika Uislamu kuna mafunzo maalum kwa ajili ya kumtendea yatima, kwa sababu amemkosa mmoja kati ya wazazi wake au wote wawili, kwa kuzingatia kuwa wazazi ni upande ambao unampa yeye upole na huruma, na kwa sababu hiyo Uislamu unaamuru yatima atendewe muamala maalumu ili yatima huyu aleleke katika mazingira ya huruma ya Kiislamu, anasema (swt):

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ

**"Ama yatima usimwonee!" (Surat Dhuhaa: 9).**

Kama mwanadamu ataleleka katika mazingira ya mabavu ya kibabe na kikatili, hakuna yeyote anayemjali au kumhurumia, mwanadamu huyu hawezi kutarajia isipokuwa njia ileile aliyoishi utotoni mwake. Anaweza kuwa na hisia ya kulipiza kisasi kwa jamii na mazingira yanayomzunguka, na ataamiliana kwa moyo mgumu na wa ubabe. Na kwa sababu hii utaukuta Uislamu unatahadharisha uwepo wa hali ya ufakiri, kuhitajia na dhulma katika jamii, hiyo ni kutokana na yale yanayozalishwa na mazingira haya ikiwa ni pamoja na visasi vibaya dhidi ya jamii, na kwa ajili hiyo imepokewa katika hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kuwa amesema: "Ufakiri unakaribia kuwa ni ukafiri." [6] Kama ambavyo Abu Dhar al-Ghiffari ana neno zuri katika hilo, anasema: "Pindi ufakiri unapokwenda katika mji ukafiri huuambia nichukue na mimi pamoja nawe." [7]

[6] Al-Kafiy, Juz.2, chapa ya 14055 Hijiria (Beirut Daaru Taaruf) Uk. 307.
[7] Shiat Fil- Mizan, chapa ya nne 1399 Hijiria (Beirtu Daaru Taaruf), Uk. 364

# MAAMKIZI YA UISLAMU

Na kwa kuwa Uislamu unahimiza mwanadamu kuishi katika mazingira ya utamaduni wa amani na salama, kwa ajili hiyo umeweka sharia ya kuanza kuamkia kwa salamu: Asalam alaykum. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema: "Hakika salamu ni jina miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi lisambazeni baina yanu." [8] Na imepokewa kutoka kwake: "Mtu bakhili zaidi ni bakhili wa salamu." [9] Na imekuja kutoka kwa Abu Ja'far al-Baqir (as) kwamba amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anapenda kutoa salamu." [10] Na mafunzo ya Uislamu yanahamasisha kuanza kutoa salamu ambapo yameifanya kuwa ni sunna. Na imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwamba amesema: "Kusalimia ni sunna na kujibu salamu ni wajibu."[11] Kwa salamu mwanadamu anatuma ujumbe wa matumaini kwa anayekutana naye na kana kwamba anamwambia: Hutopata kutoka kwangu isipokuwa kheri.

Hivi ndivyo Uislamu unavyoandaa utamaduni kwa mwanadamu, ambapo anakuwa ameandaliwa kwa amani na kusaidiana pamoja na wengine katika maisha yake, na utamaduni huu unamsukuma katika kuwafikiria wengine na sio kutia mkazo katika ubinafsi wake tu. Mkabala wa hilo ni utamaduni wa mabavu, utamaduni unaomfanya mwanadamu awe mbinafsi mwenye kujizingira katika dhati yake tu na raghaba zake na wala hajali mambo ya wengine, utamaduni huu unaandaa mazingira ya ubabe kwa mwanadamu kwa sababu hajali

[8] Jaamiu Ahaadiyth Shiah, Juz. 20, chapa ya kwanza 1416 Hijiria (Qum tukufu), Uk. 118, Hadith ya 12.

[9] Mirizaa Husain cha Nuuri Tabrisiy katika Mustadrakul- Wasail, Juz. 8 chapa ya tatu 1991 (Beirut Musasati Aalil Bait liihiyaai turathi), Uk.358, Hadith ya 1.

[10] Jaamiu Ahadiyth Shiah, Juz. 20, Uk.116 hadith ya 1.

[11] Wasailus-Shiah, Juz.12, Uk. 58.

wengine na anajali nafsi yake tu, na maslahi yake yanaweza kupelekea kuwafanyia wengine uadui.

Hapa kuna mas'ala muhimu: Utamaduni wa Kiislamu unamlea mwanadamu katika kutozingatia nafsi yake tu, bali inapasa nafsi yake kuwazingatia na wengine pia:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

**"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na hisani na kuwapa jamaa na anakataza uchafu na uovu na dhulma. Anawapa mawaidha ili mpate kukumbuka." (Surat Nahli: 90).**

Yaani kuwafanyia watu wema, na katika hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Viumbe ni waja wa Mwenyezi Mungu anayependeza zaidi kwake ni mwenye manufaa zaidi kwa waja wake."[12] Mafunzo haya yanamwelekeza mwanadamu kwamba utamu mkubwa anaoustahiki sio tu kutimiza raghaba zake binafsi bali ni ule utamu wa kimaanawiya ambao unapatikana katika kuwahudumia wengine.

Na aliulizwa mmoja wa Maulamaa wema: Kama haitabakia katika umri wako isipokuwa saa moja tu utaitumia wapi? Akasema: "Nitakaa katika mlango wa nyumba yangu nikimsubiria mwenye haja ili nimkidhie haja yake, na hili ndio tunda la mafunzo ya Uislamu."

Na katika Qur'an Aya nyingi zinamwelekeza mwanadamu kuzingatia haja za wengine bali Qur'an inahimiza kupendelea wengine:

[12] *al-Mujaazati Nabawiyah* (Qum: Mashuraati maktabatu Baswiratiy), Uk. 241.

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"Na waliofanya maskani na imani yao kabla yao, wanawapenda waliohamia kwao wala hawapati dhiki katika vifua vyao kwa walivyopewa, na wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu. " (Surat Hashir: 9).**

Na Qur'an inatupa mfano bora kutoka katika sira ya Ahlulbayt (as) ambao ni kigezo chema kwetu. Anasema (swt):

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا

**"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na mateka. Hakika tunawalisha kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu tu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani." (Surat Insaan: 8 - 9).**

Aya hii inasimulia kisa maarufu[13] kutoka kwa Ahlulbayt (as), familia kamili ambayo watu wake ni watu wa funga: Ali, Fatma, Hasan na Husein (as) na mtumishi wao. Walifunga na wakati wa kufuturu walitoa chakula chao chote kwa maskini na kulala na njaa. Na katika siku ya pili walimpa yatima na katika siku ya tatu anawajia mateka, na katika siku ya tatu wanatoa chakula chao kwa wengine

[13] Kwa ukamilifu wa kisa rejea tafsiri *Majimaul- Bayaan*, Juz. 10, Uk. 209 na Biharul-An'war, Juz. 35, Uk. 245.

kwa kuwapendelea wao, na kwa ajili hiyo Qur'an imedumisha tukio hili tukufu.

Na katika historia ya Uislam kuna matukio mengi yenye utamaduni kama huu, katika moja ya vita vya Kiislam, mmoja wao amesema: Nilikwenda kuangalia majeruhi na nilikuwa na maji, nikamwendea mtoto wa ami yangu nikamwambia: Nikupe maji ya kunywa? Akatikisa kichwa akiashiria kukubali. Mara akamsikia mwingine analalamika kwa maumivu akisemaa: Aah! Aah! Basi akaniashiria niondoke niende kwa yule mwenye kulalamika. Nikamwambia: Nikunyweshe maji? Akatikisa kichwa chake kwa kukubali, mara naye akamsikia mtu mwingine akilalamika kwa maumivu Aah! Aah! Basi naye akaniashiria niondoke na kwenda kwa yule mwenye kulalamika. Nikamwendea nikakuta ameshafariki, nikamrudia mtu wa pili nikakuta ameshafariki, nikamrudia mtoto wa ami yangu naye pia nikakuta ameshafariki.[14]

Hivi ndivyo tunavyokuta kina cha kuwapendelea wengine kwa masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).

Utamaduni huu unamfanya mwanadamu ajizuie kuwafanyia wengine ubaya katika damu zao au roho zao au mali zao. Katika hadith kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Mwislamu ni yule ambaye watu wanasalimika kutokana na mkono wake na ulimi wake."[15]

Katika upande mwingine hakika utamaduni wa Qur'an unazingatia kumfanyia mtu mmoja ubaya ni kuwafanyia ubaya wanadamu wote:

[14] *Tafsir Qurtubiy*, Juz. 18 chapa ya kwanza 1420 Hijiria. (Beirut Daarul – Kutubi al- Ilimiya), Uk. 28.
[15] *Swifat Shiah* (Teheran kanun intisharaati A'bidiy), Uk. 31.

مِنْ أَجْلِ ذَٰلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِنْهُمْ بَعْدَ ذَٰلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ

**"Kwa ajili ya hayo tukawaandikia wana wa Israil ya kwamba atakayeua nafsi isiyoua nafsi au kufanya ufisadi katika ardhi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kuiokoa ni kama amewaokoa watu wote. Hakika waliwafikia mitume wetu kwa hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika ardhi." (Surat Maidah: 32).**

Na katika hadith kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Hakika kuondoka dunia yote ni jambo jepesi kwa Mwnyezi Mungu kuliko damu inayomwagwa pasi na haki."[16]

Utamaduni huu unalea katika kuchunga na kuheshimu haki za wengine na kutowafanyia ubaya, amesema (swt):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحَرِّمُوا طَيِّبَاتِ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiharamishe vizuri alivyowahalalishia Mwenyezi Mungu. Wala msipetuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaopetuka mipaka." (Surat Maidah: 87).**

[16] *Tahadhibul- Kamaal*, Juz. 9, chapa ya nne 1413 Hijiria (Beirut Muasasatu Risala), Uk. 237, na *Kanzul- Ummal*, Hadith ya 39947.

Imepokewa katika hadith kutoka kwa Abu Abdillahi (as) amesema: "Mwenye kushiriki hata kwa neno moja tu katika kumwaga damu iliyoharamishwa, siku ya kiyama atakuja ameandikwa baina ya macho yake: Mwenye kukata tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu."[17]

Na katika riwaya ni kwamba Nabii (saww) baada ya kukamilisha amali za Mina alisimama mbele ya Waislamu na akasema: "Enyi watu! Ni siku gani hii?" Wakasema ni siku tukufu, kisha akasema: "Ni mwezi gani huu?" Wakasema ni mwezi mtukufu, akasema: "Enyi watu ni mji gani huu?" Wakasema: Ni mji mtukufu, akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameharamisha kwenu damu zenu, mali zenu na kuvunja heshima yenu, kama ulivyo utukufu wa siku yenu hii, katika mwezi wenu huu na katika mji wenu huu hadi siku mtakayokutana naye."[18]

---

[17] *Kanuzul- Ummal*, chapa ya tano 1405 Hijiria (Beirut Muasasatu risala), Hadith ya 39935.
[18] *al- Khiswaali*, chapa ya kwanza 1429 Hijiria (Beirut Darul- Murtadhaa), Uk. 487

# UTAMADUNI WA ZAMA ZA KIMADA

Na kinachosikitisha ni kwamba binadamu leo hii wanaishi katika kivuli cha utamaduni unaozalisha ubabe na kulea ukatili, utamaduni huu wa kimaada ambao unatilia mkazo ubinafsi na kuchochea matamanio ya mwanadamu  na raghba zake, na unaandaa mwelekeo huu kupitia matangazo kwa njia mbalimbali ambazo zinaunga mkono mwelekeo huu.  Utamaduni huu ambao unatukuza ubabe na mabavu unapanda mwelekeo huu kwa watu na hasa watoto, kupitia filamu za katuni ambazo nyingi kati yake zina utamaduni wa mabavu na mafunzo ya ukatili.

Zaidi ya hapo ni kwamba vitendo vya mabavu, ukatili, umwagaji damu, na mauaji holela havipingwi kama ilivyokuwa katika wakati uliopita. Kila siku katika  matangazo ya habari mwanadamu anaona maiti, mauaji na uharibifu, mwonekano huu ambao katika wakati uliopita mwanadamu alikuwa anaanguka kwa kusikia tu achia mbali kuona, leo  umekuwa ni jambo lenye kuzoeleka na la kawaida kwa mdogo na mkubwa, mwonekano huu  unazalisha ubabe na ukatili na kuutangaza katika jamii. Na kwa sababu hiyo jamii mbalimbali zinakabiliwa na ukatili na makosa ya jinai.

Katika kila sekunde mbili na nusu Marekani kunatokea kosa la jinai. Na yanatokea matukio zaidi ya elfu tano ya makosa ya jinai ndani ya Marekani yaliyopangiliwa. Katika matokeo ya utafiti uliyofanywa katika kundi kubwa la Wamarekani walioulizwa: Ni matatizo yapi makubwa ambayo mnakabiliana nayo? Asilia 21 walijibu: Ni makosa ya jinai ya ukatili na utumiaji nguvu. Na asilimia 40 ya Wamarekani wanalazimika kubadilisha muundo wa maisha yao kwa kuogopa kufanyiwa makosa ya jinai na kwa kuogopa waovu.

Jamii yetu kwa kuizingatia kuwa ni sehemu ya ulimwengu huu na inaunganishwa kupitia vyombo vya habari na mawasiliano ya kijamii, na sisi tumekuwa tunaishi na matatizo kama haya katika jamii zetu.

# UTUMIAJI NGUVU NA KUTISHIWA KWA AMANI YA JAMII

Hali ya mabavu inapokuwa ni ya kawaida kwa watu, na wanapowatukuza wenye ubabe badala ya kusimama pamoja na anayedhulumiwa, hapa amani ya jamii huwa katika hatari. Wakati ambapo utamaduni wa Kiislamu unaamuru jamii kushikamana pamoja na aliyedhulumiwa na kumshutumu dhalimu, Qur'an tukufu inaendelea milele kulaani dhulma iliyotokea kabla ya maelfu ya miaka, kosa la jinai walilotendewa kundi la waumini pasi na haki, anasema (swt):

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ وَالْيَوْمِ الْمَوْعُودِ وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ
قُتِلَ أَصْحَابُ الْأُخْدُودِ

**"Naapa kwa mbingu yenye Buruji! Na kwa siku iliyoahidiwa! Na kwa shahidi na chenye kushuhudiliwa! Wemelaaniwa watu wa mahandaki." (Surat Buruji: 1- 4).**

Hivi ndivyo Qur'an inavyoonyesha tukio hili kwa ukubwa huu. Na sisi tunapokumbuka mateso na dhulma iliyotokea kwa Ahlulbayt hakika ni kwa ajili ya kuimarisha nguzo hii, nayo ni:  Kushikamana pamoja na waliodhulumiwa.

Na mkabala wa hili kuna utamaduni unaowatukuza madhalimu na wala haupingi wanayoyafanya miongoni mwa dhulma, na anapokufa dhalimu inamtosheleza shahada mbili.

Na katika baadhi ya vitabu vya turathi tunakuta baadhi ya maneno ya kushangaza, katika kitabu cha Tahadhib, kwa mfano kuna

riwaya kutoka kwa Umar bin Sa'ad na katika maelezo inasemwa juu yake kwamba: "Umar bin Sa'ad ni taabi'i mkweli, alimuuwa Husein."[19] Kana kwamba kosa la kumuuwa Imam Husein si chochote wala halipelekei kuporomosha uaminifu wa mwenye kulitenda!!

## AMANI YA JAMII YETU INAELEKEA WAPI?

Amani ya jamii ni maudhui muhimu sana, mwanadamu anatarajia kuishi katika jamii ambayo humo anapata amani katika nafsi yake, mali yake na heshima yake, na hili ni jambo muhimu katika furaha ya mwanadamu. Katika riwaya kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) anasema: "Neema ya duniani ni amani na afya ya mwili. Na neema iliyo kamilifu akhera ni kuingia peponi."[20]

Katika wakati uliopita amani katika jamii yetu ilikuwa inapatikana kwa wingi, watu walikuwa na amani katika nafsi zao, nyumba zao, familia zao, na mali zao. Ndiyo, haikuwa ni jamii ya malaika hivyo yaliweza kutokea makosa, wizi na uovu, lakini kuna taofauti baina ya kuwa hali hizi ni za mtu mmoja mmoja  na ni chache, na baina ya kuwa nyingi na kukaribia kuwa ni hali ya kawaida. Mwanadamu anashangaa kwa anayoyasikia baina ya wakati mmoja na mwingine miongoni mwa uovu dhidi ya nafsi, heshima na mali, hadi inakaribia tusisadiki kwamba haya yanayotokea katika jamii yetu ambayo tulikuwa tunajifakharisha nayo na tunajivunia mbele ya umma zingine. Matukio katika nyanja hii ni mengi na miongoni mwayo ni: Kuwafanyia mabaya wanawake kwa kuibiwa mikoba yao, kuwaudhi wakati wakitembea barabarani na sokoni, na vile vile kuwafanyia mabaya watoto kwa kuwateka, na kuwafanyia mabaya

[19] Baadhi ya watu wa Hadith wamepinga ukweli wa Umar bin Sa'd miongoni mwao ni  Ibnu Mu'in ambapo amesema: " Vipi aliyemuuwa Husain atakuwa ni mkweli?" *Tahdhibut-Tahdhib*, Juz. 7, Uk. 396.

[20] *Maanil- Akhibaar*, chapa ya 1379 Hijiria (Qum  Muasasatu Nashiril- Islaamiy), Uk. 408.

wafanyakazi wa kike wanaoletwa ambao hapo nyuma walikuwa wanahisi utulivu kwa kuwa kwao wafanyakazi katika sehemu hii. Baadhi ya makosa haya yanaarifiwa na vyombo vya habari na magazeti ya ndani, jambo ambalo linatia mkazo kwamba tunaishi katika hali ya hatari yenye kutisha, na ni wajibu tutangaze sote hali ya hatari na tuangalie upya utamaduni wetu na mfumo wetu wa mafundisho yetu, na vile vile utekelezaji wa vyombo vya usalama na mahakama. Hali hii inazidi kuongezeka katika jamii yetu, nilimuuliza mmoja wa viongozi katika upande husika je yanayotangazwa katika majarida ni jambo lililotiwa chumvi? Akanijibu: "Bali yanayotangazwa ni sehemu ndogo tu katika yanayotokea katika jamii."

Na taarifa za kimataifa zinaashiria kwamba nchi bora zaidi katika ulimwengu iliyofaulu kupunguza idadi ya makosa ni Japani, sababu ni nini ?

Utafiti unasema: Sababu ni wingi wa taasisi za vijana Japan, ambapo kuna taasisi 540 elfu zinazojali vijana, moja ya taasisi hizo jina lake ni Umoja wa Vijana wa Uongozaji na Uelekezaji, katika umoja huo kuna vijana 126 elfu wenye kujitolea miongoni mwa vijana, na kuna taasisi za wanawake za uwezeshaji zinazohusika na wanawake tu, na humo kuna wanawake 360 wenye kujitolea.

Uwepo wa taasisi ambazo zinashughulika na vijana na kuwavutia ni jambo la dharura, na linalosaidia kupunguza ongezeko la makosa katika jamii. Na ni wajibu wetu kutumia fursa ya uwepo wa vijana katika majilisi za Husein ili kuwaelekeza vijana na kuhamasisha jamii kuwa na mfano wa taasisi kama hizi. Kama ambavyo ni wajibu wetu tusifurahie sana mengi yanayotokea katika Ashura katika kuamiliana na maadhimisho, ikiwa tu hatujayatumia katika kurekebisha nyendo za kijamii, hakika kuamiliana huku kunatubebesha jukumu kubwa nalo ni kutoghafilika na yanayotokea katika jamii, kila mmoja ni mwenye jukumu, na vyombo vya usalama vina jukumu

lake navyo vinatakiwa vitoe juhudi za ziada, ni sahihi kwamba vinashughulika na kupambana na ugaidi, lakini wananchi wanatarajia dauru kubwa zaidi katika kulinda amani ya jamii, na upande wa mahakama vilevile ni juu yake uwe mkali zaidi katika kutoa hukumu, kwa sababu wapuuzi (waovu) wanapohisi kuwepo kwa ulaini hakika hilo linawasukuma kufanya makosa na kutojali adhabu. Inapasa onyo liwe kwa kiwango kinachotakiwa ambacho anastahili muovu, na sio kuwa laini kwa wakosaji na kuruhusu misamaha, kwani sisi tuko katika kipindi ambacho tunahitaji ukali.

## IMAM HUSEIN ALISHIKAMANA NA AMANI KATIKA MAPAMBANO YAKE:

Kwa nini Imam Husein (as) alifanya harakati? Je, katika mapambano yake alikhalifu mfumo wa amani?

Hakika Imam Husein (as) amefanya harakati kwa ajili ya kuhifadhi umma na kulinda maslahi yake, na aliona kwamba utawala wa Ban Ummayya hautoi amani kwa watu bali unafanya mabaya dhidi yao, na tayari Amirul-Muumina Ali bin Abi Twalib alikuwa ameshasema kuwahusu Bani Ummayya: "Wallahi wataendelea hivi mpaka wafikie kiasi cha kuwa hawatoacha alichokiharamisha Mwenyezi Mungu ila watakihalalisha, wala ahadi ila wataitengua, na hata haitobakia nyumba ya matofali wala ya manyoya ila dhulma yao itaingia, na ubaya wa matendo yao utawafanya duni, mpaka watakuja kusimama waliaji wawili: Mliaji analia kwa ajili ya dini yake na mliaji analia kwa ajili ya dunia yake."[21]

[21] *Nahjul- Balagha,* Sharhu ya Muhammad Abduh, chapa ya kwanza 1409 Hijiria (Beirut: Daarul-Balagha) khutba ya 98.

# BAINA YA UKHALIFA NA UFALME

Umma huu ambao ulikuwa unaishi katika kivuli cha ukhalifa ambao ulimalizika kwa kufa shahidi Amirul-Muuminina Ali bin Abi Twalib (as), ghafla ulishuhudia Yazid akijitangaza kuwa ni Amirul-Muuminina! Imam Husein (as) alishikamana na mkataba wa suluhu ambayo aliifanya Imam Hasan (as) pamoja na Muawaiya, licha ya kwamba upande wa pili ulivunja mkataba na kufanya ubadhirifu na uharibifu katika Baitul-Mali ya Waislamu, kwani Muawiya alitangaza hayo alipowahutubia Waislamu kwa kusema: "Sikuwapiga vita ili mfunge, mswali, mtoe zaka na mhiji, najua mnafanya yote hayo, bali nimewapiga vita ili niwatawale na Mwenyezi Mungu amenitawalisha juu yenu hali yakuwa nyinyi ni wenye kuchukia."

Na hapa naashiria kwenye kitabu kizuri cha mwanafikra wa Kiislamu na mlinganiaji maarufu naye ni Sheikh Abu al-A'laa Maudud, naye ni kati ya maulamaa wakubwa wa Kiislamu katika zama hii, aliyepata tuzo ya mfalme Faiswal kwa ajili ya kuutumikia Uislamu mwaka 1997. Mwanachuoni huyu ana kitabu muhimu sana jina lake ni Ukhalifa na Ufalme?[22] humo anazungumzia juu ya ukhalifa ambao ulimalizika kwa kuuliwa Imam Ali (as) na anaulinganisha na ufalme muovu ulioanzishwa na Ban Ummayya. Abu al-A'laa anaashiria katika kitabu chake kwamba dola ya Ban Ummayya hakika iliasisiwa kwa sababu ya mazingira ambayo yaliandaliwa na uzembe ambao ulizunguka ukhalifa wa Uthman.

Kuna baadhi walioudhika kutokana na kitabu hiki kwa sababu ya kumkosoa kwake sahaba, al-Maudud amesema kwa jibu la ufafanuzi ambalo ameliambatanisha katika chapa ya pili, nayo tayari imeshasambazwa, ameashiria humo kwamba kumheshimu sahaba

[22] *Abu al-Alaa al-Maudud*, chapa ya kwanza 1398 Hijiria (Kuwait: Daarul- Qalam).

hakuzuii kupata zingatio katika maisha yao, wala haimaanishi tunyamazie makosa, kunyamaza kwetu kutakuwa ni sharia itakayofuatwa na watu.

Na vilevile kuna kitabu cha Muhammad Qutub naye ni mwanachuoni maarufu wa Misri aliyeishi Saudia na ameshiriki katika kuandaa mitaala ya kidini anwani yake ni: Vipi tutaandika historia ya Kiislamu, humo anasema: "Katika ambalo hakuna shaka ndani yake ni kwamba historia ya kisiasa kwa Waislamu ni mbaya sana, kutokana na yale yaliyomo katika historia yao yote. Hakuna shaka kwamba umetokea upotovu mwingi katika nyanja za kisiasa katika mfumo wa Kiislamu wa asili, na upotovu huu umetokea mapema katika historia ya Kiislamu, na haikuwa inapasa kutokea."[23]

Na cha kushangaza katika jambo la Yazidi ni kwamba yeye alikuwa anafanya uovu wake chini ya anwani ya Uislamu, Ibnu Kathir anasema katika al-Bidayah Wanihayah kuhusu Yazid bin Muawiya: "Ana mambo mazuri miongoni mwa ukarimu, upole, ufasaha, ushairi, ushujaa na rai nzuri katika ufalme, na pia alikuwa anaelemea kwenye matamanio na kuacha baadhi ya swala katika baadhi ya nyakati, na wakati mwingi akiziacha kabisa."[24]

Na vilevile anapokea Ibnu Kathir: "Kwamba Yazid alikuwa ni mashuhuri kwa kucheza ngoma, kunywa pombe, kuimba, kuwinda na kucheza kwake na vijana, watumwa na mbwa, na kupiganisha madume ya kondoo, dubu na nyani, na wala hakuna siku isipokuwa alikuwa ni mlevi, na alikuwa anamfunga nyani kwenye farasi kwa kamba na kumkokota, na anamvalisha nyani kofia za dhahabu na vile vile vijana, na alikuwa anashindanisha baina ya farasi, na ilikuwa anapokufa nyani anamhuzunikia."[25]

[23] *Kaifa Nakutubu Taarikhal- Islamiy*, chapa ya kwanza 1412 Hijiria (Cairo Daaru Shuruuq), Uk. 16.

[24] *al- Bidayah Wanihayah*, Juz. 8, chapa ya kwanza 1421 Hijiria (Beirut: Daarul- kutubi al- ilimiya), Uk. 239.

[25] Rejea iliyotangulia, Juz. 8, Uk. 244

Huyu ndio Amirul-Muuminina!!!!

Na makubwa zaidi kuliko yaliyotangulia, ni Muawaiya alipotaka kumfanya Yazid kuwa makamu wake alimhutubia kwa kusema: "Ewe mwanangu kuna uwezekano mkubwa ulioje wa kufikia haja yako bila ya kufanya uovu unaoondoa utu wako na uwezo wako." Kisha akasoma mashairi:

"Shughulika mchana kwa kutafuta matukufu, na subiri kumhama kipenzi wa karibu, hadi usiku utakapoleta kiza, na likafumba jicho la mwenye kuangalia, basi fanya usiku unayoyataka, hakika usiku ni mchana wa waovu. Ni mafasiki wangapi unawahesabu kuwa ni wachamungu, ameshafanya mmoja wao maajabu usiku. Usiku umemfunika kwa pazia lake, akawa katika amani na maisha mazuri, na ladha ya mpumbavu iko wazi, anakwenda mbio kwayo kila adui muovu."

Na hata Muawiya alipomtaka ushauri Ziyad bin Abiihi katika jambo la Yazid, yeye alimshauri ampe muda huwenda mwendo wa Yazid utabadilika na ikawa kuna uwezekano wa kuuzika (kwa watu). Riwaya ya kihistoria anayoipokea al- Ya'qubiy katika Taarikh yake[26] inasema: "Hakika Ibn Ziyad alimwambia Muawiya: 'Watu watasemaje tutakapowaita katika kutoa kiapo cha utii kwa Yazid ilihali yeye anacheza na mbwa na nyani, anavaa dhahabu na ametopea katika kunywa pombe, na anacheza ngoma. Na mbele yake yupo Husein bin Ali, Abdillahi bin Abbas, Abdillahi bin Zuberi, Abdillahi bin Umar. Mwamrishe afuate tabia ya hawa mwaka au miaka miwili, huwenda tutamsitiri kwa watu."

Huyu ndiye Yazid mwenye kucheza na nyani, mnywa pombe mwenye kutangaza ufuska hadharani, muuwaji wa nafsi isiyo na hatia na mwishowe anakuwa Amirul-Muuminina. Alisema kweli

---

[26] *Tarikh al-Yaaqubiy*, Juz. 2, chapa ya 1384 Hijiria (Najafu: Manshuraati al- makitabati al- Haidariya), Uk. 220.

mshairi wa Ahlulbayt Sayid Ja'far al-Hilliy alipoelezea hali yake kwa kauli yake:

"Sijajua mashujaa wa Kiislamu walikwenda wapi, na namna gani Yazid amekuwa mfalme baina yao, mnywa pombe mwenye kulaumiwa kwa aina yake, na kutokana na tabia mbaya inayomuwia vigumu muovu."

Kwa sababu hiyo Imam Husein alitangaza msimamo wake tangu siku ya kwanza katika nyumba ya Walid Gavana wa Madina alipomtaka kutoa kiapo cha utii, pale aliposema: "Ewe kiongozi hakika sisi ni Ahlulbayt wa Mtume na chimbuko la ujumbe na mahala pa kuteremkia malaika, kwetu Mwenyezi Mungu amefungua na kwetu amehitimisha, na Yazid ni mtu fasiki, mnywa pombe, muuwaji wa nafsi isiyo na hatia, mwenye kutangaza ufasiki bayana, na mtu mfano wangu hawezi kumpa kiapo cha utii mtu aliye mfano wake."[27]

[27] *Aluhuf Fiy Qatilah Tufuuf*, chapa ya kwanza 1417 Hijiria (Qum: Anuwaarul- Hudaa), Uk. 17.

# HUSEIN NA MAPAMBANO YA AMANI:

Imam Husein (as) alipojua jambo hilo alifanya harakati za kuelimisha umma ili ubebe jukumu lake, alitangaza harakati zake za amani za mabadiliko bila ya kutumia silaha na akasema neno lake mashuhuri ambalo linabainisha sababu ya kutoka kwake: "Hakika mimi sikutoka kwa shari wala kwa kiburi wala kwa kufanya uharibifu, wala kwa dhulma bali nimetoka kwa ajili ya kutaka kuleta marekebisho katika umma wa babu yangu, nataka kuamrisha mema na kukataza maovu na kwenda kwa mwendo wa babu nyangu na baba yangu."[28]

Na kweli Imam alishikilia msimamo wake, lakini Yazid hakusikiliza hilo, akaamuru kikosi kiende Makka na kumuuwa Imam Husein (as) hata kama atakuwa ameng'ang'ania Kaaba. Na katika sehemu nyingi Imam Husein (as) alitangaza kwamba harakati yake ni ya amani na sio ya vita, na miongoni mwa sehemu hizo ni msimamo wake pamoja na Hurru Riyahiy ambaye alikuja na maelfu ya wapiganaji waliobanwa na kiu,[29] walisimama mbele ya Imam (as) wakati wa adhuhuri katika jua na Imam (as) akawaona na walikuwa wamekaribia kuhiliki kutokana na ukali wa kiu, na ilikuwa ni fursa nzuri kwa Imam (as) kuwapiga vita na kuteka mali zao, lakini aliwahurumia kutokana na hali yao na akawafumbia macho, ilihali anajua kwamba wao wamekuja kwa ajili ya kumpiga vita na kumwaga damu yake, na japo baadhi ya wafuasi wake walimshauri juu ya hilo lakini mfumo wa Imam haukuwa hivyo na wala hauko hivyo, hiyo ni kwa sababu nembo yake ni: "Hakika mimi nachukia kuwaanza wao kwa

[28] *Mausu'atu Kalmaatil- Imamil- Husain*, chapa ya tatu 1417 Hijiria (Qum: Daarul-Ma'aruf), Uk. 354.

[29] *Hayatul – Imami Husain bin Ali*, Juz. 3, chapa ya kwanza 1413 Hijiria (Beirut Daarul-balaagha), Uk. 74.

vita."[30] Kisha akaamuru wafuasi wake kuwanywesha maji wao na farasi wao.

Hapa Imam Husein (as) anatia mkazo kwa umma kwamba haipasi kutumia ubabe na silaha katika kubadilisha siasa; kwa sababu hiyo sio katika masilahi ya jamii, na Maulamaa na Mafaqihi wetu wameshazungumza kuhusu upande huu na miongoni mwao ni Marjaa Marehemu Sayyid Muhammad Shiraziy ambaye ameandika katika nyanja hii vitabu vingi kuhsu "Hakuna kutumia nguvu katika Uislam"[31] na kuhusu "Usalama na Amani",[32] na humo ametilia mkazo kwamba hakuna nafasi ya kulazimisha rai na kuwatawala watu kwa silaha na nguvu, na kwamba vitendo hivi sio katika Uislamu. Na kwa masikitiko makubwa katika zama zetu hizi Uislamu na Waislamu wamepakwa matope kwa sababu ya vitendo vya kigaidi ambavyo haviutakii Uislamu na Waislamu kheri, na kwa sababu yake umma umekosa amani yake na utulivu wake na haikubaki nchi yoyote kati ya nchi za Waislamu isipokuwa imedhurika kwa vitendo hivyo.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aunusuru umma na shari ya fitina hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

[30] *Biharul- An'waar*, Juz. 45, Uk. 5.
[31] *Alaa U'nfu Fiyl – Islaam*, chapa ya kwanza 2002 (Beirut Daarul- Ilimi).
[32] *As-Silim Wasalaam*, chapa ya kwanza 1426 Hijiria (Beirut daarul- ilim).

# IMAM HUSEIN NA MFUMO WAKE KATIKA KULINGANIA NA KUJADILIANA

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Surat Nahli: 125).**

## NJIA YA KUATHIRI WENGINE

Ni jambo la kawaida mwanadamu kuikuta nafsi yake katika maisha haya mbele ya anayehitalifiana naye katika rai, na ambaye maslahi yake yanapingana na maslahi yake. Watu wanatofautiana katika rai zao na mielekeo yao, na kila mmoja kati ya watu anataka kumiliki kiasi kikubwa zaidi kadiri iwezekanavyo katika chumo katika dunia hii, jambo linalosababisha aina ya mgongano katika maslahi baina ya watu. Na mwanadamu anapokuwa mbele ya anayemkhalifu katika rai hakika anaweza kwenda mbio ili kumkinaisha kwa rai yake, ama kutokana na hali ya kidini, kwa kuzingatia kwamba dini inamsukuma muumini kumhubiria mwenzake mafunzo ya dini yake, na nususi zilizopokelewa zinatilia mkazo hilo, kutoka kwa

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Mwenyezi Mungu kumuongoa mtu kupitia mikono yako ni bora zaidi kwako kuliko vilivyochomozewa na jua au vilivyochoewa na jua."[33]

Na katika baadhi ya nyakati inajitokeza hali ya ubinafsi kwa mwanadamu wakati wa kwenda mbio kueneza rai zake, kwa kuzingatia kwamba ni aina ya ushindi wa dhati na kwa hivyo anajikuta ni mwenye kujawa na sururi na furaha. Na swali muhimu hapa ni: Ni ipi njia ya kuathiri wengine? Na ni vipi nitahifadhi maslahi yangu wakati yanapogongana na maslahi ya wengine?

Kuna njia mbili:

## KWANZA: KUTUMIA NGUVU NA KULAZIMISHA:

Hapa mwanadamu hurejea kwenye nguvu ili kulazimisha rai yake, hakika kulazimisha fikra na rai sio sahihi na haiwezekani, kama ambavyo wewe una akili basi na mwingine pia ana akili, anaweza kutofautiana na wewe katika fikra, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba watu wakiwa huru, hivyo haisihi kwa yeyoye kulazimisha rai yake kwa wengine hata kama atakuwa anaitakidi kwamba rai yake ni ya haki na ni sahihi, ambapo kila mtu anaitakidi kwamba rai yake ni ya haki na ni sahihi, na itikadi hii haitoi kisingizio cha kulazimisha rai kwa wengine, Mwenyezi Mungu Mtukfu ambaye ndiye Mlezi wa viumbe halazimishi watu kumwamini kwa nguvu na mabavu, anasema (swt):

[33] *Al- Kaafiy*, Juz. 5, Uk. 28, Hadithi 4.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَآمَنَ مَنْ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا أَفَأَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّى يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

**"Lau angelitaka Mola Wako, wangeliamini wote waliomo ardhini. Basi je wewe utawalazimisha watu wawe Waumini?" (Surat Yunus: 99).**

Na vile vile Manabii na Mitume ambao wanabeba ujumbe wa haki kwa watu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hawakuruhusiwa kulazimisha daawa yao kwa wengine kwa nguvu, bali kazi yao inaishia katika kufikisha:

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ وَعَلَيْكُمْ مَا حُمِّلْتُمْ وَإِنْ تُطِيعُوهُ تَهْتَدُوا وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ

**"Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Kama mkikengeuka basi yaliyo juu yake ni aliyobebeshwa, na yaliyo juu yenu ni mliyobebeshwa. Na mkimtii yeye mtaongoka na hapana juu ya mtume ila kufikisha (ujumbe) wazi wazi." (Surat Nuru: 54).**

Na pia anasema:

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيْطِرٍ

**"Basi kumbusha hakika wewe ni mkumbashaji tu. Wewe si mwenye kuwatawalia." (Surat Ghashiya: 22).**

Ikiwa Mitume na Manabii hawana haki ya kulazimisha rai ya haki na ujumbe wa haki kwa watu je, inasihi kwa yeyote kufanya kazi hii?

Lakini baadhi ya wenye kiburi wanakwenda mbio ili kulazimisha rai kwa nguvu, na katika historia yetu ya Kiislamu tunakuta namna gani baadhi ya watawala walikuwa wanakwenda mbio juu ya hilo. Na kwa hakika hiyo sio ikhilasi kutoka kwao, kwa rai hizo, lakini ni kitendo cha ubabe na kuwakandamiza watu, na hawatosheki kutawala miili ya watu tu bali wanataka pia kutawala fikira zao na kudhibiti rai zao. Na hapa tunataja mfano mmoja:

al-Mahdiy al-Abbasiy ambaye alitawala umma wa Kiislam miaka 11 (kuanzia 169 - 185 Hijiria) alitengeneza katika utawala wake nembo ya kukabiliana na wazandiki, nao ni wale ambao wana rai yenye kupinga Uislamu, lakini ni namna gani alikabiliana nao? Mapambano hayakuwa kwa mantiki, majadiliano na hoja, lakini ni kwa mapanga. Tuhuma yoyote ikimfikia dhidi ya yeyote kwamba ni zandiki alikuwa anaamuru kuuliwa, na kwa siasa hii ikawa kuna mwanya wa kufitinisha na kukomoana, inatajwa kwamba waziri wake Abu Ubaydullahi Muawiya bin Yasaar alikuwa ni mwanafasihi mjuzi, naye ni mtu wa kwanza aliyeandika kitabu katika mapato, ilitokea hali ya kutoelewana baina ya waziri huyu na Rabi'i aliyekuwa mlinzi, hivyo mlinzi akataka kumkomoa, akamfitinisha kwa al-Mahdiy kwamba waziri wako ana mtoto jina lake ni Muhammad, naye anatuhumiwa katika dini yake. al-Mahdiy akasema: "Niletee." Alipoletwa akasema: "Ewe Muhammad: Soma Qur'an." Akasoma vibaya kwa kuzingatia kuwa yeye ni kijana, na kwakuwa ni mbele ya khalifa akakanganyikiwa na hakuweza kusoma vizuri. al-Mahdiy akamgeukia baba yake na kumwambia: "Ewe Muawiya je, hukuniambia kwamba mwanao amehifadhi Qur'an?" Akasema: Ndio nilikwambia, ewe kiongozi, lakini yeye ametengana na mimi

miaka mingi na katika muda huu amesahau Qur'an." al-Mahdiy akasema: "Simama jikurubishe kwa Mwenyezi Mungu kwa damu yake." Akasimama ili afanye hivyo lakini akaanguka. Mmoja kati ya wahudhuriaji akaingilia kati, naye ni Abbasi bin Muhammad, akasema: "Ewe kiongozi ukipenda msamehe mzee." Akafanya hivyo, lakini bado al-Mahdiy aliamuru mtoto wake akakatwa kichwa." [34]

Njia hii haikubaliwi na akili wala dini, sasa ni ipi njia ya sawa?

**Pili: Ni Kuathiri Wengine kwa Njia ya Majadiliano na Kukinaisha:**

Nayo ndio njia inayoamrishwa na Qur'an tukufu, anasema (swt):

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ وَجَٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦ ۖ وَهُوَ أَعْلَمُ بِٱلْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Surat Nahli: 125).**

**Hekima:** Inatokana na udhibiti, nayo ni kuweka kitu mahala pake, unapotaka kumkinaisha mtu chagua maneno yanayofaa, hoja inayofaa na njia inayofaa, na hekima inamaanisha kuisemesha akili kwa dalili.

**Mawaidha mazuri:** Inamaanisha kuathiri utu na hisia nzuri, kiasi kwamba mawaidha hayawi makali.

---

[34] Daulatul- Abbasiya 1970, (Cairo maktabatu tijaariya), Uk. 89.

Na inawezekana upande mwingine una shubuha, hivyo kuwa tayari kupokea rai yake na jadili pamoja naye, huu ndio uongofu wa mbinguni na maelekezo yake, kujadili na kuzungumza pamoja naye kwa njia bora zaidi na mazungumzo mazuri Zaidi: **“Na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora.”**

## TATIZO LA MAJADILIANO KATIKA JAMII YA KIISLAMU

Sisi tunaona katika zama hizi kwamba jamii zilizoendelea zimekata masafa ya ukomavu katika muamala wake wa ndani pamoja na matatizo yake ya kifikira, kisiasa na katika maslahi mablimbali, wao wanahitalafiana lakini wanajadiliana na wanazungumza na hatimaye wanafikia kwenye ufumbuzi na wanaishi pamoja na ikhitilafu zao mbalimbali katika nyanja na medani mabalimbali. Ama katika jamii yetu ya Kiislamu, jamii hii ambayo ilikuwa ni wajibu iwe ndio mfano katika uhusiano wake wa ndani kwa mafunzo ya Aya ya Qur’an Tukufu:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

**“Mmekuwa ni umma bora mliotolewa kwa watu, mnaamrisha mema na kukataza maovu na mnamwamini Mwenyezi Mungu.” (Surat Aali Imran: 110).**

Tunaikuta hali yetu haiakisi hali hiyo yenye kuangaza ambayo Qur’an inaitaka kwetu, na kwa hiyo unakuta jamii zetu zinaishi ka-

tika matatizo mbalimbali katika nyanja hii, na matatizo haya yako aina mbili:

Matatizo yenye kulipuka na mengine ni kama vile moto chini ya majivu unaweza kulipuka wakati wowote, kwa nini?

Kwa sababu sisi hatufuati njia ya mazungumzo, na hii inaweza kuwa ni katika athari za kasumba za kijahilia, kinyume na mwongozo wa Uislamu, ambao miongoni mwa mafunzo yake ni: Usamehevu na kuheshimiana kwa pande zote. Lakini athari za kasumba za kijahilia bado hazijamalizika. Na wakati mwingine inatokea fitina na matatizo na mizozo bila ya kisingizo wala sababu.

Imenukuliwa kuhusu moja ya vita vikubwa katika historia ya Waarabu kwamba mtu alinyoosha mguu wake katikati ya njia na akapiga kelele: "Yeyote ambaye ni mwanaume basi asogeze mguu wangu kutoka kwenye njia hii." Mmoja wa wapita njia hakuweza kuvumila maneno haya akachukua upanga wake na akakata mguu wake. Na kwa sababu ya tukio hili dogo ikatokea vita ya kipumbavu baina ya makabila mawili kutokana na kitendo cha kipumbavu.

Na katika hali yetu ya kijamii wakati mwingine tunaona baadhi ya matatizo na tunapoingilia ili kuyatatua tunakuta kwamba sababu yake ni ya kipuuzi haistahiki kutokea tatizo kwa sababu yake. Na unakuta hali hii imeenea katika jamii yetu ya Kiislam na ya Kiarabu katika nyanja na viwango tafauti, sawa iwe ni katika ngazi ya familia au katika siasa au katika mambo ya kijamii au katika nembo ya kimadhehebu, na kwa hiyo utaona katika nchi za Waislamu kama vile Afghanistani, Palestina, Lebanoni, Iraki, Somalia na Sudani kuna matatizo mengi na mizozo mingi.

Swali: Kwa nini matatizo haya yamerundikana katika jamii ya Kiislam na ya Kiarabu? Wakati ambapo tunakuta upungufu wa kiwango cha matatizo katika jamii zingine, je wao si wana mgongano katika maslahi vilevile?

Ndiyo, na maslahi huko ni makubwa sana kuliko yalivyo katika jamii zetu za Kiislamu na za Kiarabu. Na tunawakuta wanatofautiana na maslahi yao yanagongana, kinachowatofautisha na sisi ni kumiliki kwao mfumo wa kuamiliana pamoja na matatizo yao. Na sisi kwa masikitiko makubwa hatuna mfumo huu. Na hata nchi yetu haiepukani na aina hii ya matatizo ya kijamii ambayo hayana kisingizio, tarehe 18/12/1412 Hijiria, nilisoma (katika jarida) habari mbili kuhusu mambo mawili tofauti:

**Habari ya Kwanza:** Inazungumzia kuhusu mzozo uliotokea katika mji mmoja wa Saudia, kuna watu ambao ilitokea baina yao ikhitilafu kuhusu makaburi, habari inasema: Kwamba waombolezaji wawili walizozana wakati wa kusindikiza jeneza, kwa sababu ya mvutano tu baina ya wachache miongoni mwao yalitokea mapigano baina yao na kusababisha baadhi yao kujeruhiwa kwa majeraha mbalimbali.

Na sababu ya lililotokea inarejea katika mabishano yaliyotokea baina ya watu wawili kati ya waombolezaji, mabishano yaliyotokana na ikhitilafu ya zamani iliyokuwepo baina yao, hivyo ikageuka kuwa mapigano ya mikono; kisha baadhi ya waliokuwepo wakaingilia kati na mzozo ukawa mkubwa hadi zikatumika fimbo na makaburi yakageuka uwanja wa mapigano, mpaka chombo cha usalama kikaingilia kutuliza ghasia, na mapigano yakasababisha kujeruhiwa watu wanne huku mmoja akijeruhiwa vibaya sana.

Pamoja na kujua kwamba mwanadamu anapokuwa makaburini inampasa akumbuke mauti na hisabu na auweke moyo wake katika unyenyekevu, lakini hili halikutokea, na kama alivyosema mshairi wa zamani: “Hakika vita mwanzo wake ni maneno.”

**Habari ya Pili:** Ilichapishwa na jarida siku ileile kuhusu mji wa Habari, inazungumzia ikhitilafu iliyogeuza hafla ya harusi kuwa

maombolezo kwa sababu ya ikhitilafu baina ya watu wa bibi harusi na watu wa bwana harusi, na damu zikamwagika na furaha ikageuka huzuni na ikamalizikia katika kituo cha polisi.

# HALI GANI HII YA KUTOKUENDELEA?

Hujitokeza hali ya ikhitilafu ya wazi upande wa kimadhehebu, na kati ya matukio ya mwisho ni mkutano wa Doha wa kuleta ukuruba baina ya madhehebu za Kiislamu, [35] pamoja kwamba mkutano ni wa kuleta ukuruba, lakini tumekuta hali ya kutoelewana iliyo wazi katika baadhi ya khutuba ambazo zilitolewa katika mkutano huo. Hakika kuwepo mkutano huu ni bora zaidi kuliko kutokuwepo, na uwazi ni njia ya kujuana na kuweka wazi picha ya wote, na hii ni bora kuliko kubakia katika ikhitilafu zilizofichikana ndani ya nafsi na wote kuishi katika hali ya kujizuia na kutokukaribiana.

Na kama nilivyoeleza, hakika watu na makundi katika jamii zilizopevuka wanapokhitalifiana wanakutana na kujadiliana ili wafikie kwenye ufumbuzi, na wanaafikiana juu ya nukta za ushirikiano, wakati ambapo katika jamii ambazo hazimiliki upevu huu hakika ikhitilafu baina ya watu wake inapelekea kutengana na kuwa mbali. Na hapa tunataja tukio lilitokea katika historia ya Waarabu kwa Nabii wetu Muhammad (saww) kabla ya utume, na umri wake mtukufu ulikuwa ni miaka 35, Waarabu walipotaka kujenga upya Kaaba na ikatokea baina ya makabila ikhitilafu kuhusu ni kabila lipi litapata utukufu wa kuweka jiwe jeusi katika sehemu yake. Ikhitilafu hii ilikaribia kuleta vita yenye kuhilikisha kama si mmoja wa wahenga kuwashauri wamfanye hakimu mtu wa kwanza atakayeingia katika msikiti mtukufu, na wakaafikiana juu ya hilo, na wa kawanza kuingia kwao alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), walipomuona wakasema:

[35] Muutamaru Dauha lilitaqriyb bainal – Madhaahib al- Islamiya ulioandaliwa na chuo kikuu cha Qatar pamoja na chuo kikuu cha Azhar cha Misri na Majimaul- A'alamiy liltaqriyb Bainal Madhaahibil- Islamiya ya Iran tarehe 20 -22 Januari 2007 sawa na tarehe 3- 5 Muharram 1428 Hijiria katika mji mkuu wa Qatar Doha.

Amekuja mkweli na mwaminifu, tumemkubali kuwa ni hakimu wetu, hapo wakamweleza tatizo. Akasema nileteeni shuka kubwa na jiwe likawekwa humo, kisha akasema: Kila kabila lishike ncha ya shuka, wakanyanyua hadi walipokaribia sehemu ya jiwe, akalichukua Mtume wa Mwenyezi Mungu na akaliweka katika sehemu yake.

Matatizo hayashindikani kutatuliwa akili inapopewa fursa ya kuingilia katika jambo. Na leo umma wetu wa Kiislamu unaishi katika matatizo ya kimadhehebu ya kiubaguzi ambayo yanatakiwa kulipuliwa katika wakati huu mgumu. Na kama suala lingekuwa katika mikono ya wenye akili jambo lingekuwa jepesi sana, isipokuwa uwanja umeachwa kwa wachupa mipaka na wenye kasumba, Zaidi ya hapo ni uwepo wa matakwa ya kimaslahi, na kisiasa yanayotaka kulipua hali ya umma na kuushughulisha na tatizo hili. Vinginevyo hakika madhehebu sio mapya na ikhitilafu za kimadhehebu ni jambo la kihistoria tangu karne kumi na nne, na nilikuwa nawaambia baadhi ya Maulamaa wa Kisuni: Kila tatizo ambalo mnalo dhidi ya madhehebu ya Shia ni la zamani, na majibu ambayo tunayo ni ya zamani walishayasema Maulamaa wetu, sasa hadi lini tutabaki katika hali hii ya upofu?

Hapa unajitokeza umuhimu wa majadiliano na ukuruba. Kwa nini tuwe mbali? Na kwa nini tutuhumiane? Na kwa nini tuache fursa kwa maadui ili wanufaike kutokana na hitilafu hizi kwa hisabu ya maslahi yetu, utukufu wetu na mustakabali wetu?

Hapa Maulamaa katika zama hizi wamezungumza kwa sauti ya akili na mantiki, miongoni mwao ni Sheikh Ali Abu al-Hasan al-Khaniziy (r.a) (aliyezaliwa mwaka 1291 Hijiria na kufariki mwaka 1363 Hijiria) ambaye alitunga kitabu *Daawatul-Islamiyah Ilaa Wahdat Ahali Sunnat Wal-Imamiyah*[36] ambacho kina ukubwa wa zaidi ya kurasa elfu moja.

[36] Sheikh Ali Abu al- Hasanal- Khaniziy katika *Da'awatul- Islamiya Ilaa Wahdati Ahali Sunna wal- Imamiyah*, chapa ya kwanza 1422 Hijiria (Beirut: Sharkatu Daaru al- Mustafaa liihiyai turaath).

Na vilevile Sheikh Muhammad Swalehe bin Sheikh Ali bin Sheikh Suleiman Aali Sheikh Mubaraka (aliyezaliwa mwaka 1318 na kafariki mwaka 1394 Hijiria) ambaye alikuwa Kadhi katika mji wetu kuanzia mwaka 1376 Hijiria hadi kufariki kwake, yaani muda wa miaka kumi na nane. Ana kitabu jina lake ni *Daawat Fiy Kalmati Tawhid*,[37] humo alifuata njia ya kuleta ukuruba baina ya Waislamu na kuwalingania kwenye kufahamiana wao kwa wao kabla ya yeyote kuelekeza tuhuma ovu kwa ndugu zake, kwa kutilia mkazo umuhimu wa umoja katika kila hali, kila wakati na kila sehemu.

Ni haja ilioje ya sauti ambazo zinazungumza kwa sauti ya akili na mantiki ili tutatue mambo kwa majadiliano na sio kwa mashambulizi na malumbano. Ni wajibu wetu tufahamu mambo vizuri, malumbano haya ya ukinzani yatatufikisha wapi? Sisi ni watu wa nchi moja na sote tuko katika lengo moja, kwanini tunatoa fursa kwa maadui? Na tatizo kubwa ni kwamba athari za uchochezi zinadhihiri katika maisha ya wananchi na katika uhusiano wao na wengine pindi wanapokutana katika sehemu mbalimbali kama vile idara za serikali, vyuo vikuu, shuleni na sehemu nyingine za umma, na hii ni hatari kubwa, ni wajibu wetu kuiepusha nchi yetu isije kutumbukia humo.

[37] Sheikh Ali Abu al- Hasanal- Khaniziy katika *Da'awatul- Islamiya Ilaa Wahdati Ahali Sunna wal- Imamiyah*, chapa ya kwanza 1422 Hijiria (Beirut: Sharkatu Daaru al-Mustafaa liihiyai turaath).

# DONDOO KUTOKA KATIKA RIWAYA YA IMAM HUSEIN (AS) NA SIRA YAKE

Watu wengi wanamjua Husein (as) kwamba ni mwenye kudhulumiwa na wanajua mateso na machungu ambayo aliyabeba, nayo ni makubwa na ni muhimu. Lakini sisi ni wajibu tujue vilevile kuhusu mafunzo ya Imam Husein (as) na mfumo wake katika upande wa kulingania na majadiliano. Miongoni mwa maneno yake (as) ni kwamba alisema: "Usizungumze yasiyokuhusu, hakika mimi naogopa kwako dhambi, wala usizungumze kuhusu yanayokuhusu hadi uone mahala pa kuyazungumzia, huwenda mzungumzaji amezungumza kwa haki lakini ikawa ni aibu kwake. Wala usijifaharishe kwa mpole wala kwa mpumbavu, hakika mpole atakudharau na mpumbavu atakuudhi." [38]

Na katika ibara zifuatazo kuna baadhi ya dondoo kutoka katika sira ya Imam Husein (as) kuhusu maudhui tunayozungumzia.

[38] Sheikh Muhammad Swalehe Aali Sheikh Mubaraka al- Khatwiy as Swafuwaaniy katika *Da'awat Fiy Kalmat Tawhid* chapa ya kwanza 1422 Hijiria (Beirut sharkatu Daarul-Mustafaa liihiyaai turathi).

# WEREVU WA KUKOSOA

Unapomuona mwanadamu mwenye kukosea katika rai yake au katika vitendo vyake inapasa kujaribu kumuongoza lakini kwa werevu, baadhi ya watu hawana mbinu nzuri utawaona wanatumia onyo na kemeo haraka, na hili ni kosa.

Hebu tutafakari msimamo huu kutoka katika sira ya Imam Husein: Walipita maimamu wawili Hasan na Husein (as) wakati wangali wadogo, kwa mzee aliyekuwa anatawadha, na hakuwa akitawadha vizuri. Jukumu hapa linahitajia kumwelekeza na kumuongoza, na kwa kuzingatia kuwa ni mtu mzima mkubwa kwa umri na wao ni wadogo walifikiria njia ya werevu kwa namna ambayo hawatausononesha utu wake na hisia zake, kwani lengo ni kuelekeza, alikwenda mmoja wao kwake na kusema: "Ewe mzee kuwa hakimu baina yetu kila mmoja wetu atatawadha." Wakatawadha kisha wakasema: "Nani kati yetu anatawadha vizuri." Akasema: "Nyote mnatawadha vizuri isipokuwa huyu mzee mjinga ndio ambaye hakuwa anatawadha vizuri, na sasa amejifunza kutoka kwenu na ametubia mbele yenu kwa baraka zenu na huruma yenu kwa umma wa babu yenu." [39]

[39] *Biharul- An'war, Juz*. 75, Uk.127 Hadith ya 10.

# KUEPUKANA NA MIJADALA ISIYO NA TIJA

Imepokewa kwamba mtu alimwambia Imam Husein (as): "Kaa ili tujadiliane katika dini." Akasema: "Ewe mtu, mimi najua dini yangu na najua uongofu wangu, kama wewe hujui dini yako basi nenda ukaitafute, ni wapi mimi na majadiliano!! Hakika shetani anamshawishi mtu na anamnong'oneza na kumwambia: Jadiliana na watu katika dini ili watu wasihisi mapungufu yako na ujahili wako."[40]

Na hili ni somo kubwa, na ni wajibu tulitafakari, hakika mwanadamu inapasa asivutike kwenye mjadala usio na tija. Na napenda kutoa angalizo kwamba maneno haya ya kiubaguzi ya kimadhehebu ambayo yamejaa anga yanataka kushughulisha watu na mijadala tasa. Nasaha yangu kwa nafsi yangu na kwa ndugu zangu wananchi wote ni kwamba wajiepushe kuingia katika mjadala huu. Wakati mwingine unaona katika madrasa au chuo kikuu au katika sehemu yoyote mjadala unaotokana na yale wanayoyasikia katika runinga, na baadhi wanadhani kwamba ni wajibu wake kujitetea, na kama hajajadili atakuwa dhaifu, na kutokana na mantiki hii baadhi wanatumbukia na kuvutika katika mjadala huu tasa, ambao haujulikani utaishia wapi. Asidhani yeyote kwamba kwa kujibu kwake anatumikia madhehebu na itikadi, dhana hii ni makosa.

Na mara nyingi lengo la upande mwingine la mjadala ni uchochezi na kutengeneza tatizo, tumeshuhudia na tumesikia mengi katika nyanja hii, na kwa sababu hii Qur'an inawasifu waumini kwa kauli yake (swt):

[40] Rejea iliyotangulia, Juz.43, Uk. 319.

وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا

**"Na wale ambao hawawi kwenye uzushi, na wanapopita kwenye upuzi hupita kwa heshima zao." (Surat Furqan: 72).**

Na kauli yake (swt):

وَعِبَادُ الرَّحْمَٰنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا

**"Na waja wa Mwingi wa rehema ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu. Na wajinga wakiwasemesha, husema: ‹Salama.›" (Surat Furqan: 63).**

Kama tungesoma vitabu vya Hadithi kama vile *al-Kafiy* na *Biharul-An'war* tungekuta riwaya nyingi kutoka kwa Maimamu wetu (as) kuhusu majadiliano, mazungumzo na kujionyesha katika dini, nazo ni hadithi zinazokataza hali hiyo, Imam as-Sadiq (as) anasema: "Jihadharini na ugomvi katika dini hakika unazizuia nyoyo kujishughulisha na utajo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu."[41] Na nasema: "Msigombane na watu kwa ajili ya dini yenu hakika ugomvi unaleta ugonjwa katika nyoyo, waacheni watu hakika watu wamechukua kutoka kwa watu."[42]

Na ni wazi kwamba wewe huwezi kubadilisha ukinaikaji wa wengine; kwa sababu wao wamechukua maarifa yao kutoka kwa masheikhe wao wanaowazingatikia kuwa ni watukufu na wanawaheshimu. Na kuna riwaya kutoka kwa Imamu al-Baqir (as) ambayo inatia mkazo juu ya dharura ya kuwa mbali na mjadala na majadil-

[41] *Biharul- An'war*, Juz. 2, Uk. 128 hadith 6
[42] *Biharul- An'war*, Juz. 2, Uk. 133 hadith 24

iano tasa, inawaeleza Mashia kwa sifa ya ajabu, Imam anasema: “Hakika Mashia wetu hawazungumzi.”[43] Ikimaanisha kujiepusha kwao na hali hii isiyo na faida.

Hadi mmoja wa wanafunzi wa Imam as-Sadiq (as) alimwambia Imam: “Imenifikia kwamba wewe umechukia kujadiliana na watu.” Akasema: “Ama maneno ya aliye mfano wako hayachukiwi, ambaye akiruka anajua kutua vizuri bila kuanguka, na akitua anajua kuruka vizuri, ambaye yuko hivi hatumchukii.”[44] Na amesema Abdul-Ulaa: Nilimwambia Abu Ja’far: “Hakika watu wanamtia dosari Ali kwa maneno, na mimi najadiliana nao.” Akasema: Ama mfano wako, ambaye anatua kisha anaruka, huyu ni bora, ama anayetua lakini hawezi kuruka, huyu hapana.”[45]

Hapa tunatia mkazo kwamba mtu yeyote ambaye ana uwezo wa kutatua mambo kwa njia sahihi inasihi kwake kujadili, ama ikiwa hawezi hayo kama ikiwa maarifa yake ni madogo au hawezi kudhibiti hasira zake basi mjadala sio katika maslahi yake na madhehebu hayanusiriwi kwa mjadala bali yananusurika kwa amali njema.

[43] *Biharul- An’war*, Juz. 2, Uk. 135 hadith 33
[44] *Biharul- An’war*, Juz. 2, Uk. 136 hadith 39
[45] *Biharul- An’war*, Juz. 2, Uk. 136 hadith 38

# KUAMSHA UTU, DHAMIRA NA MAADILI YENYE UONGOFU

Njiani Imam Husein alipokuwa anakwenda Iraki alipitia katika sehemu inayoitwa Zarud, na huko alikuta hema la Zuhair bin al-Yaqiin, na alikuwa ni katika watu wa Uthman yaani kati ya wanaounga mkono kutaka kulipiza kisasi kwa damu ya Uthman, hivyo msimamo wake ulikuwa umeathirika kwa msimamo wa Ban Ummayya, riwaya zinaashiria kwamba Zuhair alikuwa ameazimia kumkwepa Imam Husein (as) njiani ili asipate taabu ya kukutana naye, hivyo haikutokea kusimama msafara wa Imam Husein na msafara wa Zuhair bin al-Yaqin katika sehemu moja muda wote katika njia ya Husein (as) hadi Iraki, isipokuwa katika sehemu hii (Zarud) ambapo Zuhair hakuwa na hiyari nyingine.

Imam (as) akatuma mjumbe kwake akimwita aende kwake, mpokezi amesema: Sisi tulipokuwa tumekaa tunakula, ndipo alipoingia mjumbe wa Husein akasalimia, na akasema: "Ewe Zuhair bin al-Yaqin hakika Abu Abdillahi Husein bin Ali amenituma kwako nikwambie uende kwake." Mpokezi anasema: "Kila mtu alitupa kilichokuwa mkononi mwake kana kwamba imetuteremkia balaa." Mke wake akamwambia: "Je, Mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu anatuma kwako mjumbe kisha huendi? Subhanallah, lau ungemwendea usikie maneno yake!!" Zuhair bin al-Yaqiin akamwendea, haukupita muda akaja hali ni mwenye furaha na uso wake umebadilika na kuwa wa njano, akaamuru apewe tandiko lake na vitu vyake akavibeba kuelekea kwa Husein, kisha akamwambia mke wake: "Wewe umeachwa! Nenda kwa Ahali yako, hakika mimi sipendi upate kwa sababu yangu isipokuwa kheri." Kisha akawaambia wafuasi wake: Anayependa miongoni mwenu anifuate, hakika haya ni maagano ya mwisho.

Na katika riwaya nyingine: "Anayependa kufa shahidi miongoni mwenu basi asimame na anayechukia basi aondoke. Hakika mimi nitawasimulia hadithi; Tulipigana vita (Balanjar) na Mwenyezi Mungu akafungua kwetu na tukapata ngawira, Salman al- Farisiy akasema: "Mmefurahi kwa aliyofungua Mwenyezi Mungu kwenu na mliyoyapata miongoni mwa ngawira?" Tukasema: Ndio, akatuambia: Mtakapo mkuta kijana wa Aali Muhammad – na katika riwaya nyingine: Bwana wa vijana wa Aali Muhammad – basi kuweni ni wenye furaha zaidi kwa kupigana kwenu pamoja nao kushinda ile ya yale mliyoyapata miongoni mwa ngawira. Ama mimi nawaaga." Mke wake akamwambia: Mwenyezi Mungu amekuchagulia, nakuomba unikumbuke siku ya kiyama mbele ya babu wa Husein (as)."

Na katika riwaya nyingine ni ule msimamo aliouonesha Husein (as) kwa adui mkubwa, ambaye aliongoza jeshi dhidi ya Husein, naye ni Umar bin Sa'd, pamoja na uadui huo utamkuta Imam Husein (as) katika siku ya tisa ya Muharram anataka kukutana na Ibn Sa'd, lakini Ibn Sa'd anakataa, mwishoni anaafiki, riwaya inasema:

Husein alimwambia: "Ole wako, ewe Ibn Sa'd! Je humuogopi Mwenyezi Mungu, nakuona unanipiga vita na unataka kuniuwa, na mimi ni mtoto wa ambaye umeshamjua, waache hawa watu, waache wao na kuwa pamoja na mimi, hakika hilo liko karibu zaidi na wewe na ni lenye kukurubisha kwa Mwenyezi Mungu." Akamwambia: "Ewe Husein, hakika mimi naogopa kuvunjiwa nyumba yangu huko Kufah na kuporwa mali zangu." Husein alimwambia: "Mimi nitakujengea nyumba bora kuliko nyumba yako." Akasema: "Naogopa kuchukuliwa mifugo yangu huko Sawadi." Husein akamwambia: "Mimi nitakupa miongoni mwa mali zangu Baghibaghah, nayo ni chemchem kubwa iliyopo katika ardhi ya Hijazi, Muawiya alitaka kunipa thamani yake dinari milioni moja

za dhahabu na sikumuuzia." Umar bin Sa'd hakukubali chochote kati ya hayo.

Husein aliondoka kwwake akiwa amekasirika na akisema: "Mwenyezi Mungu akuchinje haraka ewe Ibn Sa'd juu ya kitanda chako, na wala asikusamehe siku ya kufufuliwa kwako, wallahi hakika mimi nataraji hutakula katika ngano ya Iraki isipokuwa kidogo sana." Umar bin Sa'd akamwambia kwa istihizai: "Ewe Husein, hakika kuna shairi badala ya ngano."[46]

Huu ndio mfumo wa Husein na sira yake, inafaa kwa umma uchukue katika mfumo huu wa kiutume ambao unaangazia njia ya maendeleo na mafanikio.

[46] *Hayatul- Imamil – Husain*, Juz. 3, Uk. 133.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani

167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi

188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)

209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique